| MSANII KUINGIA NCHINI | |
|---|---|
| **HUDUMA** | **KIBALI** |
| Kibali cha kawaida kwa msanii wa Afrika Mashariki | TShs 1,000,000 |
| Kibali cha kawaida kwa msanii asiye wa Afrika Mashariki | TShs 1,500,000 |
| Kibali cha dharura kwa msanii yeyote kuingia nchini | TShs 2,500,000 |

| MATUKIO YA SANAA | |
|---|---|
| **HUDUMA** | **KIBALI** |
| Kibali kwa matukio ya kibiashara | TShs 2,000,000 |
| Kibali kwa matukio yasiyo ya kibiashara | TShs 200,000 |
| Kibali kwa matukio yasiyo ya kibiashara yenye kiingilio | TShs 1,500,000 |


| GHARAMA ZA KIBALI KWA KUMBI ZA MAONESHO YA SANAA NA BURUDANI: (ZISIZO ZA FILAMU) | | | |
|---|---|---|---|
| **HUDUMA** | **USAJILI** | **KIBALI** | **JUMLA** |
| Zenye Ukubwa wa kukaa watu wasiozidi 350 | TShs 50,000 | TShs 350,000 | TShs 400,000 |
| Zenye Ukubwa wa kukaa watu 351 - 550 | TShs 50,000 | TShs 550,000 | TShs 600,000 |
| Zenye Ukubwa wa kukaa watu 551 - 750 | TShs 50,000 | TShs 750,000 | TShs 800,000 |
| Zenye Ukubwa wa kukaa watu 751 na kuendelea | TShs 50,000 | TShs 1,050,000 | TShs 1,100,000 |

| GHARAMA ZINGINE | GHARAMA JUMLA |
|---|---|
| Kampuni kutumia wasanii kwenye Tangazo (Kila Tangazo) | TShs 5,000,000 |

**FAHAMU:**

Usajili haulipiwi kila mwaka

Kibali hulipiwa kila mwaka




**Kwa mawasiliano zaidi**

Katibu Mtendaji

Jengo la Utumishi

8 Barabara ya Kivukoni

S.L.P 4779 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 222 863 748

Barua pepe: info@basata.go.tz

Tovuti: www.basata.gotz

**basata.tanzania**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

BARAZA LA SANAA LA TAIFA - BASATA

NATIONAL ARTS COUNCIL



## MFUMO WA USIMAMIZI WA TAARIFA ZA MSANII

Artist Management Information System - AMIS) kwa sasa Baraza linatoa huduma ya usajili na vibali kwa wasanii na wadau wake ambao ni wasajiliwa wapya na waliosajiliwa kupitia mfumo huu wa kielektroniki kwa wasanii binafsi, Vikundi vya wasanii, Vyama, Mitandao ya Wasanii Mashirikisho ya Wasanii, Taasisi, Kampuni, Studio za kurekodi muziki na kumbi za sherehe, Harusi na burudani wataweza kuhuisha taarifa zao kupitia huduma nyinginezo.

## HATUA ZA KUJISAJILI

1. Fungua Browser (Mfano Firefox, Chrome, Internet Explorer)

2. Katika sehemu ya anuani ya mtandao andika https://sanaa.go.tz

3. Utakuja ukurasa wa mfumo wa Wadau wa Sanaa

4. Kwa mtumiaji ambaye hajasajiliwa atabonyeza eneo ambalo limeandikwa JISAJILI, itatokea fomu itakayomtaka aingize taarifa zake.

5. kwa kuanza na Barua pepe, jina la kwanza, kati na ukoo, atachagua jinsia, atachagua tarehe yake ya kuzaliwa akisha kamilisha vyote atabonyeza sehemu iliyoandikwa Endelea, itatokea kisanduku chenye ujumbe kikielezea

6. Umetumiwa ujumbe kwenye barua pepe yako. Ataingia kwenye barua pepe yake atakutana na

7. Ujumbe unaosema AMIS REGISTRATION utafungua tena ujumbe na kukutana na kisanduku chenye ujumbe wa AMIS LINK. Utabonyeza link hiyo kisha itakuelekeza kubadilisha nywila (Password) ambapo utatakiwa kuingiza nywila katika eneo la juu nakurudia nywila hiyo katika eneno la chini. Mfano Nywila Sisi.2022 nk.

8. Mtumiaji atakapo badilisha nywila (password) atabonyeza kitufe kilicho andikwa endelea. Ambapo mfumo utampa ujumbe wa kuonesha umefanikiwa kubadilisha nywila (Your Password word successful changed).

Baada ya hapo mfumo utamrudisha mtumiaji kwenye ukurasa wa mwanzo wa mfumo.

9. Katika ukurasa wa mwanzo wa mfumo mtumiaji atapaswa kuingiza barua pepe (Email Address) alisajilia awali pamoja na nywila (Password) aliyotengeneza kisha atabonyeza ingia.

10. Akifanikiwa kuingia baada ya kuingiza Barua pepe (Email Address) aliyosajilia awali pamoja na nywila (Password) kwa usahihi atachagua kisanduku chenye nembo ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Baada ya hapo atachagua eneo husika analohitaji kupata huduma. maeneo yaliyopo ni kama yanavyoonekana katika picha.

11. Mtumiaji ataendelea kutumia huduma husika atakayokuwa akihitaji kwa wakati huo kwa kuzingatia sifa na mahitaji muhimu ya huduma.

## VIAMBATANISHO KATIKA MFUMO

Viambatanisho muhimu kwa Wasajiliwa wapya

1. MSANII BINAFSI - Picha, Wasifu (PDF) na Kitambulisho (PDFY

2. VIKUNDI - Katiba, Picha ya Viongozi na Muhutasari wa kikao (PDF)

3. TAASISI/VYAMA/MITANDAO YA WASANII/ MASHIRIKISHO YA WASANII - Katiba (PDF) picha ya viongozi (PDF) na Muhutasari wa Kikao (PDF)

4. KUMBI ZA SHEREHE NA BURUDANI - Picha za kumbi (png) na kitambulisho cha mmiliki (PDF)

## GHARAMA ZA USAJILI NA VIBALI

**ZIMETUNGWA KWA KANUNI ZA BASATA ZA MWAKA 2018, CHINI YA KIFUNGU CHA 65 CHA KANUNI HIZI NA KUTANGAZWA KATIKA GAZETI LA SERIKALI LA TAREHE 9/02/2018 , NOTISI NAMBA 43**

| HUDUMA | USAJILI | KIBALI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Taasisi | 50,000 | 100,000 | 150,000 |
| Mashirikisho | 50,000 | 60,000 | 110,000 |
| Vyama | 50,000 | 50,000 | 100,000 |
| AZISE | 50,000 | 60,000 | 110,000 |
| Promotoa \| Kampuni | - | 300,000 | 300,000 |
| Makampuni yanayotumia wasanii kujitangaza | - | 500,000 | 500,000 |
| Wasanii Binafsi | 20,000 | 20,000 | 40,000 |
| Wasanii Binafsi kutoka nje ya Tanzania | 50,000 | 50,000 | 100,000 |
| Wasanii ndani ya vikundi vya sanaa | 15,000 | - | 15,000 |
| Vikundi vya Uimbaji, kwaya na kaswida | 40,000 | 40,000 | 80,000 |
| Wafanya Biashara wadogo wadogo wa kazi za sanaa | 50,000 | 60,000 | 110,000 |
| Vikundi vya sanaa | 40,000 | 40,000 | 80,000 |
| Maabara (Label) ya sanaa | 50,000 | 60,000 | 110,000 |
| Studio za kurekodia muziki usio na filamu | 50,000 | 60,000 | 110,000 |
| Mawakala/Wasambazaji wa kazi za sanaa | 50,000 | 70,000 | 120,000 |
| MaDJ | 40,000 | 50,000 | 90,000 |

## WALIOSAJILIWA TAYARI

Kwa Wasanii na Wadau waliosajiliwa (Existing Registers) ni lazima kuhuisha taarifa zako kwenye mfumo ikiwa pamoja na kujaza taarifa zake za usajili wa awali na kuweka viambatanisho kwa ombi husika